

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu 6(1) Na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA VIBAO VYA MATANGAZO YA BIASHARA)
ZA HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJJI, 2010

Jina na mwanzo wa kutumika	1	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Vibao vya Matangazo ya Biashara) za Halmashauri ya Manispaa Kigoma Ujji za mwaka 2010 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.
Eneo la matumizi	2	Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujji.
Tafsiri	3	<p>Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-</p> <p>“Afisa Muidhiniwa” maana yake ni Afisa Biashara, Mhandisi, Mkaguzi wa Halmashauri au Afisa yeyote atakayetuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.</p> <p>“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujji.</p> <p>“Matangazo ya Biashara” maana yake ni maandishi yoyote yalioandikwa na kuwekwa au kubandikwa katika maeneo au majengo yoyote katika eneo la Halmashauri kwa lengo la kutangaza Biashara au Kampuni, Ofisi au Taasisi yoyote inayohusika na biashara au kutoa huduma za Biashara.</p> <p>“Mfanyabiashara” maana yake ni mtu yeyote, Kampuni, Shirika, Taasisi, Kiwanda, chochote ambaye au ambacho anafanya biashara ya kutengeneza, kuuza, kusafirisha au kuhifadhi bidhaa katika eneo la Halmashauri.</p> <p>“Vibao vya Matangazo” maana yake ni vibao vyote vilivyo katika maeneo ya wazi au kubandikwa kwenye nyumba za Biashara au maandishi yenye kutangaza biashara.</p>
Wajibu wa mfanyabiashara	4	Itakuwa ni wajibu wa kila Mfanyabiashara, Kampuni, Shirika, Taasisi au Kiwanda kulipa ushuru wa vibao vya matangazo kwa kila Tangazo lake kwa mwaka kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Uwezo wa Afisa Muidhiniwa Makosa 5 6

Afisa Muidhiniwa anaweza kuingia katika jengo au eneo lolote wakati wa saa za kazi kugagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo;-

- (a) atamzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake;
- (b) atakayetoa taarifa za uongo;
- (c) atakataa au kukwepa kulipa ushuru;
- (d) atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu wasilipe ushuru;

7

Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi Shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela, au adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

JEDWALI

SEHEMU A

VIWANDA NA MASHIRIKA

NA.	JINA LA KAMPUNI/BIASHARA	KIWANGO KWA MWAKA
1.	Coca cola/Pepsi	300,000/=
2.	Bia	300,000/=
3.	Sigara	300,000/=
5.	Makampuni au vituo vyote vya mafuta	300,000/=
6.	Benki zote	300,000/=
7.	Posta	300,000/=
8.	Ticl	300,000/=
9.	Tanesco	300,000/=
10.	Bima	300,000/=
11.	Vodacom	300,000/=
12.	Zain	300,000/=
13.	Tigo	300,000/=
14.	Zantel	300,000/=
15.	Mashirika au Makampuni binafsi	300,000/=

SEHEMU B

BIASHARA NYINGINEZO

NA	JINA LA KAMPUNI/SHIRIKA	KIWANGO
1.	Hotel	200,000/=
2.	Nyumba za kulala wageni	100,000/=
3.	Bar	100,000/=
4.	Hospital Binafsi	100,000/-
5.	Maduka ya vifaa vya Ujenzi	100,000/=
6.	Maduka ya kawaida	50,000/=
7.	Mashine za Nafaka	50,000/=
9.	Vitabu na vifaa vya Ofisi	50,000/=
10.	Nguo na mavazi	50,000/=
11.	Kununua na kuuza mazao	50,000/=
12.	Maduka makubwa ya madawa Baridi na Kilimo	100,000/=
13.	Maduka madogo ya madawa Baridi na Kilimo	50,000/=
14.	Ushauri wa kitaalam	100,000/=
15.	Migahawa	50,000/-
16.	Grocery	50,000/=
17.	Stationary na Computer	100,000/-

SEHEMU C

(A) MATANGAZO YASIYONG'ARA


- (i) yasiyozidi mita moja za Mraba 20,000/=
- (ii) yasiyozidi mita mbili za Mraba 20,000/=
- (iii) yanayozidi mita mbili za Mraba 20,000/=

(B) MATANGAZO YANAYONG'ARA

- (i) yasiyozidi mita moja za Mraba 10,000/=
- (ii) yanayozidi mita mbili za Mraba 10,000/=

(C) MATANGAZO YA VIPAZA SAUTI 20,000/= kwa siku

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji unabandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 31 Julai, 2009
Nembo hiyo umebandikwa mbele ya



LEWIS. K. KALINJUNA

Mkurugenzi

HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI




SHABANI MAMBO

Naibu Mstahiki Meya

HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI

NAKUBALI



MHE. MIZENGO. P. PINDA
WAZIRI MKUU

DODOMA...29/7/2011